**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE SHEREHE ZA UZINDUZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2025

**KIBAHA, PWANI**

**02 APRILI, 2025**

- ***Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) - Waziri Mkuu, JMT;***
- ***Mhe. Dkt. Dotto Biteko – (Mb) Naibu Waziri Mkuu ,JMT***
- ***Mhe. Mussa Zungu (Mb) – Naibu Spika Bunge la JMT;***
- ***Mhe. Prof. EliSante Ole Gabriel– Mtendaji Mkuu wa Mahakama***
- ***Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;***
- ***Mhe. Hamza Juma - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Zanzibar***
- ***Mhe. Alhaj Abubakar Kunenge - Mkuu wa Mkoa, Pwani;***
- ***Bi. Mary Maganga - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;***
- ***Bi. Fatma Hamad Rajab - Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - SMZ;***
- ***Bw. Rashid Mchatta - Katibu Tawala, Mkoa wa Pwani;***
- ***Komredi Mwinyishehe Mlao - Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Pwani;***
- ***Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri;***
- ***Wahe. Wakuu wa Mikoa;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;***
- ***Mhe. Fatma Toufiq (Mb) – Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;***
- ***Mhe. Elibariki Kingu (Mb) – Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI;***
- ***Wahe. Wabunge na Wawakilishi wote mliopo hapa;***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya,***
- ***Viongozi wa Vyama mbalimbali vya Siasa;***
- ***Viongozi wa Dini;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Ndugu Wananchi;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ...**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa Kibaha kwa ajili ya shughuli hii muhimu ya uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2025. Kwa dhati kabisa, nampongeza Mhe, Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa JMT na Ofisi yake inayosimamia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (SMT), pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (SMZ) kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kusimamia na kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru. Hali kadhalika, ninampongeza Mhe. Abubakar Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, viongozi wenzake na wananchi wa Mkoa wa Pwani, kwa kukubali kuwa mwenyeji wa shughuli hii ya Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka 2025; na, kwa maandalizi mazuri ya hafla hii kitaifa. **Hongereni sana.**

**Ndugu Wananchi;**

Kama tunavyofahamu, chimbuko la mwenge wa Uhuru ni nia ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuweka mwenge juu ya kilele cha mlima Kilimanjaro ili kuleta matumaini pale pasipo na matumaini, upendo pale penye chuki na heshima pale palipojaa dharau. Nia hii aliitoa kwa mara ya kwanza mwaka 1959 huko New York, alipohutubia Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa. Aidha, alimteua Luteni Alexander Gwebe Nyirenda kutekeleza azma hiyo iliyoitwa "Operesheni Mwangaza", ambapo yeye na wenzake walianza maandalizi mwezi Novemba 1961 kabla ya Tanganyika kupata uhuru. Hatimaye usiku wa mkesha wa sherehe za uhuru tarehe 9 Desemba 1961, Luteni Nyirenda na wenzake waliwasha na kusimika Mwenge wa uhuru na Bendera ya Tanganyika kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro kama ishara ya kuwa huru. Kupandisha mwenge kileleni ilikuwa kwanza, ni kuonesha kazi ngumu iliyoko mbele ya kulijenga Taifa changa la Tanganyika. Pili, ilikuwa ni kuuwasha mwenge uangaze nje ya mipaka, kutoa matumaini pasipo na matumaini, upendo palipo na chuki na heshima palipo na uonevu na dharau. Wimbo mashuhuri ulioimbwa na Vijana wa halaiki hivi punde, umerudia maneno ya Baba wa Taifa kuhusu sababu na umuhimu wa Mwenge wa Uhuru.

**Ndugu Wananchi;**

Wazo la kukimbiza mwenge wa uhuru nchi nzima na kila mwaka lilitolewa na Vijana wa TANU katika kikao chao kilichofanyika tarehe 26 Juni, 1964. Lengo kuu likiwa ni kutekeleza kwa vitendo azma ya Baba wa Taifa ya kuhamasisha umoja, upendo, amani na ujenzi wa Taifa kwa kuhamasisha maendeleo. Tangu wakati huo, mwenge umekuwa ukikimbizwa katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kupitia mbio hizo hamasa kubwa imetolewa ili kuendelea kudumisha amani, na kujenga uzalendo, umoja na mshikamano. Katika kipindi chote hicho, mbio za mwenge zimekuwa na mafanikio makubwa yanayosadifu maono ya waasisi wa Taifa letu.

**Ndugu Wananchi;**

Kaulimbiu ya mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2025, inasema: ***"Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu".*** Kaulimbiu hii inalenga kuwakumbusha na kuwasisitiza Watanzania wote kutumia kikamilifu haki yao ya kikatiba ya kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu ili kumchagua Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wawakilishi, Madiwani na Masheha.

**Ndugu Wananchi;**

Napenda kuwahakikishia kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu 2025, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kusimamia, kwa dhati na kwa haki misingi ya demokrasia na kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki uchaguzi kwa uhuru, kwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kuchagua viongozi wenye sifa wanaowataka.

Ili uchaguzi mkuu uweze kufanyika kwa ufanisi, amani na utulivu, napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo yazingatiwe:

a) Kila Mtanzania mwenye sifa za kushiriki uchaguzi ahakikishe anaandikishwa

kwenye daftari la kudumu la wapiga kura, kwa mujibu wa sheria na maelekezo ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

b) Wapiga kura wanahimizwa washiriki katika Kampeni za uchaguzi ili kusikiliza wagombea wa nafasi mbalimbali wakinadi sera zao na za vyama vyao. Hii ni muhimu ili kuwawezesha kufanya uamuzi wa uhakika juu ya kiongozi anayefaa kuchaguliwa. Aidha, katika kipindi hicho ni muhimu kuhakikisha hali ya usalama, utulivu na amani inadumishwa;

c) Tunawaasa wananchi wote hususan vijana, wawe waangalifu na watu wasioitakia mema nchi yetu kwa kuepuka kutumiwa vibaya kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani. Utulivu na amani tuliyonayo ni tunu na hatuna budi kuilinda kwa nguvu zote kwa maslahi ya Taifa letu; na,

d) Wadau wote wa uchaguzi, hususan vyama vya siasa, wanahimizwa na kukumbushwa kuwa wana wajibu mkubwa katika kuhakisha kuwa uchaguzi unafanyika katika hali ya amani na utulivu, kwa kuendesha kampeni zenye staha na kuzingatia Sheria na miongozo mbalimbali ya uchaguzi.
Ikumbukwe Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 42(2) na 65; Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya Mwaka 2024; Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Na. 4 ya mwaka 2018.

**Ndugu Wananchi;**
Sambamba na ujumbe uliobebwa na kaulimbiu ya mbio za mwenge 2025, masuala mengine muhimu yatakayosisitizwa ni:-

i. Umuhimu na kuzingatia Lishe Bora kwa afya imara. Hii inaambatana na ujumbe maalum usemao "***Mtaji ni Afya Yako, Zingatia Unachokula***". Ili kuboresha na kuimarisha hali ya lishe nchini, ujumbe wa mwenge utahimiza Mamlaka mbalimbali za Serikali, Wadau wa Lishe, na wananchi wote kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni za lishe bora hususan kwa mama wajawazito, watoto na jamii kwa ujumla. Aidha ni muhimu pia kusisitiza mazoezi ya mwili kwa ajili ya kujenga afya;

ii. Mapambano dhidi ya Rushwa; yataongozwa na ujumbe usemao: ***"Kuzuia Rushwa ni Jukumu lako na Langu: Tutimize Wajibu Wetu",*** Ujumbe huu utukumbushe kuwa jukumu la kupambana na rushwa siyo la mtu mmoja bali linatuhusu wote kwa kuwa rushwa ni adui wa haki na ni kikwazo cha maendeleo na ustawi wa wananchi. Ni vema wananchi wakajiepusha na vitendo vya rushwa kwa kutokutoa, kutopokea au kuomba rushwa, hasa katika kipindi cha uchaguzi mkuu;

iii. Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI; ujumbe mahsusi wa mapambano haya ni ***"Chagua Njia Sahihi, Tokomeza UKIMWI".*** Kupitia ujumbe huu, Mbio za mwenge 2025 zitaendelea kuhamasisha wananchi kupambana na maambukizi ya VVU. Ni muhimu Watanzania wote tuzingatie kuwa, afya zetu ndio mtaji wetu. Kama nchi, hatutaweza kufikia malengo yetu ya kimaendeleo

endapo tutakuwa na jamii isiyo na afya njema. Hivyo, tunawajibika kuchukua hatua za makusudi za kutokomeza maambukizi mapya ya VVU. Aidha, tunao wajibu wa kupambana na unyanyapaa kwa WAVIU, pamoja na mila potofu na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii zetu;

iv. Mapambano dhidi ya matumizi ya Dawa za Kulevya; mapambano haya yataongozwa na ujumbe maalum usemao; ***"Kataa Dawa za Kulevya: Timiza malengo yako".*** Ni dhahiri kuwa Matumizi ya Dawa za kulevya yanaathiri sana jamii yetu, na kundi kubwa la waathirika ni watoto na vijana kati ya miaka 13 hadi 24, ambao ndio tegemeo kama nguvu kazi ya Taifa. Hali hii, inatulazimu kama Taifa kuendelea kupambana kwa nguvu zote na biashara, uzalishaji na matumizi ya Dawa za kulevya nchini; na,

v. Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Malaria; mapambano haya yataongozwa na ujumbe usemao ***"Ziro Malaria Inaanza na Mimi - inaanza na wewe, inaanza na sisi sote".*** Ugonjwa wa malaria umeendelea kuwa tishio katika jamii yetu, licha ya takwimu kuonesha kuendelea kupungua kwa maambukizi ya Malaria hapa nchini. Katika baadhi ya mikoa ikiwemo Katavi, Tabora na Kagera, kiwango cha maambukizi ya vimelea vya malaria kipo juu. Hivyo, ni wajibu wetu sote kushirikiana na Serikali kupambana na ugonjwa huu kwa kutunza mazingira, kuharibu mazalia ya mbu na kutumia vyandarua.

**Ndugu Wananchi;**

Mwenge wa Uhuru 2025 unaowashwa leo, utakimbizwa kwa muda wa siku 195, katika Mikoa 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo Serikali itafikisha ujumbe kwa wananchi na kuhamasisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kutembelea, kukagua, kuzindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi ya maendeleo. Hivyo, ninaiagiza Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa, ili waweze kutekeleza jukumu la kizalendo walilokabidhiwa la kuhakikisha kuwa wanawafikia wananchi na kuwapa taarifa sahihi kuhusu sera, mipango, miradi na mikakati ya Serikali katika kuwaletea Maendeleo.

**Ndugu wananchi;**

Ninapomalizia hotuba yangu, ninawaomba tushirikiane kuwaombea dua na sala vijana wetu tutakaowakabidhi jukumu la kukimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ili Mwenyezi Mungu awajalie afya njema wakati wote watakapokuwa wanatekeleza jukumu hili adhimu. Vilevile, nawakumbusha vijana wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kuwa, Taifa limewaamini na kuwapa jukumu hili kubwa, nyeti na muhimu. Ni wajibu wa kila mmoja wenu kulitekeleza jukumu hili kwa bidii, juhudi, nidhamu, uadilifu na maarifa wakati wote. Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru; nawasihi mkafichue vitendo vyote vya udhalimu na ubadhirifu wa fedha na mali za umma bila woga.

Baada ya kusema hayo, sasa niko niko tayari kuzindua rasmi Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka 2025.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**